س ج

في الإباضيَّةِ والصَّلاة

بالسواحيلي

حمد المعولي

الطبعة الأولى
1434هـ - 2012 م

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Baada ya kumshukuru Allah mtukufu, na kumtakia Rehma na Amani kipenzi wetu Mtume wetu Muhammad na Aali zake na Masahaba wake na kila mwenye kufuata uongofu wake mpaka siku ya malipo.

Ninachukua fursa hii kwa kuwaletea yaliyomo katika kitabu kilicho chepesi kufahamika, mafupi maelezo yake, na nyingi elimu yake, nacho ni uandishi wa ndugu yetu Ust. Muhammed Al maawaliy, basi ndugu zangu tufaidike na yaliyomo katika kitabu hichi, ama mwenye kua na suala au kutaka maelezo zaidi, anaweza kuwasiliana na wanaelimu wa kiibadhi pale walipo, au kuandika baruapepe Ibadhisafi@hotmail.com ili faida izidi iweze kupatikana kwa atakayotuma, pia ifahamike kua nimefanya baadhi ya uhakiki wa hadithi zilizotajwa

katika kitabu hichi, vile vile kila utapoona yaliyomo baina ya mabano mawili, ujue kua aghalabu ya hayo yanakua ni nyongeza yetu, na hatukufanya haya isipokua kwa kutarajia kupata mazuri yaliyo kwa Allah mtukufu katika njia ya kuifikisha Haki kwa waja wake.

Wabilahi taufiqi.

Ndugu yako

Hafidh. H. Seif Al sawafi

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Shukurani zote ni kwa Allah mtukufu, yeye ndiye Mola wa walimwengu wote, na rehma na amani ziwe kwa bwana wetu Muhammad, Nabii muaminiwa, na kwa Aali zake, na Masahaba wake watimizaji ahadi, walio wachamungu.

Baada ya hayo,,,

Ndugu zangu, pokeeni kurasa hizi tunazokuleteeni; kwani ndani yake umo ufupisho mwepesi, ulio katika mfumo wa suali na jawabu, katika yale yanayohusu dhehebu la ibadhi, basi utakuta mengi yanayohusiana na hakika zao kiujumla, na yale yanayohusiana na sala yao kiuanisho.

Tunamuomba Allah mtukufu atujaalie sisi na nyinyi kua miongoni mwa wanaosikia neno zuri na wakafuata ya wema, na atuoneshe haki na atuwezeshe kuifuata.

Na Allah ndiye msimamizi wa kuwezesha katika mema.....

YANAYOHUSU DHEHEBU LA IBADHI

1. S. Kwa nini Waislamu wa dhehebu la ibadhi wameitwa kwa jina hilo la Ibadhi?
J. Jina hilo wameitwa na wasiokua wao, nalo ni jina la kisiasa, na uhakika wake ni kunasibishwa wao na Tabii (mwanafunzi wa Masahaba) Abdullahi bin Ibadhi Tamiimy, na yeye alikua ni miongoni mwa viongozi wa kisiasa wa Dhehebu hili; kwani alikua ni mashuhuri kwa harakati zake hai za ukosoaji wa mwendo wa siasa za Bani uamaiyah (Maumawiya) kwa sababu ya kujiweka kwao mbali na Sunna (ya Mtume (s.a.w)) na mwendo wa viongozi waongofu, kama alivyojulikana (Ibn Ibadhi) kwa barua zake alizokua akizielekeza kwa Mtawala Abdulmalik bin Maruan (65– 86H, 685-705AD), barua zilizobeba ubainisho wa haki, na utetezi wa wafuasi wa kambi ya upinzani ambao yeye alikua pamoja nao.

2. S. Maibadhi walikua wakitumia jina gani kabla ya kubandikwa jina hilo (la Ibadhi)?

J. Walikua wakitumia jina la:

a. Jamaatu l-muslimiina (Jamaa waislamu)

b. au Ahlu daawah (watu wa ulinganiaji)

c. au Ahlu l-istiqaamah (watu wa msimamo madhubuti).

Basi mwanzo wa kudhihirika kwa jina la Ibadhi katika safu zao ni katika karne ya tatu ya mwaka wa kiislamu (hijiria), basi jina hilo likaenea, na kuliridhia wafuasi wa dhehebu hii[1].

3. S. Ni wapi wanachukua Maibadhi mambo ya dini yao?

J. Wanayachukua hayo katika kitabu cha Allah (Qur-ani), na Sunna ya Nabii (s.a.w), na Makubaliano ya umma. Hayo ndiyo asili kwao wao katika kuipitisha sheria, na kutokana na hayo tu kunachukuliwa dalili katika dhehebu lao, basi hakuna lolote katika Aqidah (Itikadi) au katika Fiqhi (Ibada za kimatendo) isipokua nila msingi

1. *(Ibn Ibadhi hajatupangia sisi dhehebui;basi unasibisho wetu kwake ni kwa dharura ya kubaguka misimamo yetu wakati lilipochukua kila kundi njia yake)* Imamu Saalimi

madhubuti katika Qur-ani na Sunna, au kwa yale yanayorudi humo.

4. S. Maibadhi wanashikamana vipi na sunna za Mtume (s.a.w)?
J. Maibadhi ni wenye kushikamana zaidi na sunna, na wao wako safu ya mbele katika kumfuata Mtume (s.a.w), na haya wameyahakikisha wasiokua wao katika zama tofauti, na hayo anayajua kile mwenye kutalii vitabu vyao (vya Ibadhi) na tarehe yao.

5. S. Ni kitabu gani wanachokitegemea Maibadhi katika hadithi za Mtume (s.a.w)?
J.Marejeo ya mwanzo kwa Maibadhi katika hadithi ni Musnadi wa Imamu Rabii bin Habib Alfarahidi (r.a) (80 – 180H), na ndio kitabu sahihi zaidi katika vitabu vya hadithi; kwa sababu hadithi zake ni upokezi wa daraja tatu tu, na

wapokezi wake ni waaminifu zaidi[2], basi -mara nyingi- hadithi zake ni kwa kupitia kwa Abu ubaidah Muslim bin Abi kariimah (45-150H) kutoka kwa Jabir bin Zaid Al-azdi (18-96H) kutoka kwa Sahaba (r.a), vile vile Maibadhi wanategemea vitabu vyengine vya hadithi; kwani wao wanachukua yaliyo sahihi kutoka kwa Nabii (s.a.w), hata kama wameyapokea wengine wasiokua wao.

6. S. Ni utaratibu gani wa kielimu wanaoutegemea Maibadhi?

J. Maibadhi ni maarufu kwa fahamu yao pana, pia ni maarufu kwa kuzingatia kwao ya wengine, basi

2 . Maibadhi ni watu waaminifu, basi uongo hauna mlango wa kupenya katika dhehebu lao, na hakuna khilifu baina yao katika kuthibiti kwa Musnad wa Imam Rabii (r.a), na Maibadhi hawana vitabu vingi vya hadithi, wala wapokezi wengi katika hadithi zao, na hao wahusika wa Musnad, wote ni Maimamu wakuu wa Dhehebu hili, basi umashuhuri wao na uaminifu wao na elimu yao vinatosha kuondosha shaka katika kuthibiti kwa Musnad, na katika yasiyowezekana kupatikana ni kua Wanaelimu wote wa Kiibadhi wakubaliane katika jambo lisilokua la kweli.

wao ni wenye kufuata haki tu, na kwa hivyo wanachukua dalili katika Qur-ani tukufu na Hadithi sahihi zilizothibiti kutoka kwa Mtume (s.a.w) katika vitabu vyote vya Sunna, nao wanachukua maneno ya wasiokua wao kwa amana kubwa, nao ni wenye kulipa nguvu neno lolote lile wanapoliona kua dalili yake ni yenye nguvu, bila ya kujali ni nani kalisema, na hili liko wazi katika vitabu vyao.

7. S. Kwa nini tunakuta kua tuhuma za Waislamu wa madhehebu mengine dhidi ya Maibadhi katika kwenda kinyume na sunna za Mtume (s.a.w)?

J. Kutuhumiwa Maibadhi kua wanakwenda kinyume na Sunna ni zalio la kutojua misingi ya Fiqhi ya kiibadhi, pia ni mazalio (potoshaji) ya matekeo ya kitarehe na kisiasa yaliyotokeza zamani na kuacha athari zake katika vitabu vya wengine (waiokua maibadhi).

8. S. Kwa nini dhehebu la Ibadhi halina umashuhuri kama ulivyo kwa madhehebu mengine?

J. Dhehebu la kiibadhi lilienea hapo mwanzo katika sehemu tofauti za waislamu -kama itakavyokuja-, lakini baadae kulipungua kuenea kwake; kwa sababu Maibadhi -na mbele yao yuko Abdullahi bin Ibadhi- walikua katika safu za wapinzani wa siasa ya Dola ya Bani umaiyyah (Maumawiyya), na baada yake Dola ya Abbaasiyah (Maabasiya), na kwa sababu hiyo, viongozi wa Kiumaiyyah na Kiabbaasi walilipiga vita dhehebu hili, na (kuwapiga vita) wafuasi wake, basi walifanya kila juhudi za kuwazuilia watu kuujua uhakika wa dhehebu hii[3], uhakika uliochukuliwa moja kwa moja katika kiini safi cha Uislamu, basi viongozi hao walikua wakipandikiza (kwa kukusudia) -katika fikra za watu- chuki na uchafuzi wa uhakika wa

3. Uhakika wa Dhehebu hili ni (Haki ndiyo ya kufuatwa, basi watu wanajulikana kwa Haki; na haki inajulikana kwa dalili na hoja, Allah amesema: *(Sema: Leteni dalili yenu ikiwa nyinyi ni wa kweli)* [Baqarah 111, Naml 64] wala hakusema: leteni watu wenu ikiwa nyinyi ni wakweli.

Maibadhi, na kuwabandika Maibadhi jina la Khawarij.

9. S. Dhehebu la Ibadhi limeenea wapi? Na kwa sababu gani limefifia hivi sasa?
J. Ukiongezea Omani, basi Dhehebu la Ibadhi lipo Algeria, Tunisia, Libya, Yemen, na katika baadhi ya nchi zilizoko kusini mwa jangwa la sahara, kama Tanzania, Uganda, Kenya, Ghana, Mali, na nyenginezo (kama vile Burundi, Rwanda, na Congo), na dhehebu hili lilikuwepo hapo kabla katika Iraqi, Khurasani, na miji ya Sandi[4] na miji mengine. Na kufifia kwa kuwepo Maibadhi katika baadhi ya nchi hizo (na kumalizika kuwepo kwao), ni kwa sababu ya siasa za baadhi ya dola zilizohukumu miji hiyo; kwani zilikua dhidi ya Ibadhi na wafuasi wake, kiasi cha kufikia kuwakufurisha, kuwaua kidhulma, kuchoma moto vitabu vyao,

4. Sandi ni Pakstani na kaskazini ya India (Indus Valley).

(kuliona kua ni dhehebu la taifa au kabila fulani tu) na mengine yasiyokua hayo, juu ya kua Maibadhi walipopata fursa ya kuongoza walifuata njia ya uadilifu, bila ya kubeba chuki, haakuwahipo kufungua mlango mbele ya siasa za kuwachukia wengine waisokua wao, wala hawakuwapo kufuata mwenendo mbaya (waliofanyiwa wao), bali maibadhi ni maarufu kwa kushikama na misingi ya kusameheana, na kuheshimu ya wengine, na kuwazingatia wafuasi wa madhehebu mengine kua ni ndugu katika dini, (nchi, na jamii), na kutowalazimisha kufuata dhehebu lao kwa nguvu.

10. S. Kwa nini wengi hawajui mazuri ya Maibadhi, tarehe yao, na vitabu vyao?
J. Hayo ni kwa sababu ya mazalio ya kasumba, dhulma, uhasidi, na mazushi mabaya, na (mara nyengine inafikia hata) kulazimishwa Maibadhi kuacha dhehebu yao, hayo yamotokeza katika zama tofauti za

tarehe, (na mpaka leo fatwa za kuwakandamiza Maibadhi zinatoka kidhulma dhidi ya Ibadhi).

11. S. Kwa nini, uongo mwingi na uzushi dhidi ya Maibadhi na dhehebu yao umeenea katika madhehebu mengine?

J. Yameenea hayo, kwa sababu ya dhulma za viongozi na watawala waliouhukumu kidhulma Umma huu wa kiislamu katika zama za mwanzo, na kwa sababu ya siasa zao za kijeuri, na kumpiga vita kila mwenye kusimama dhidi ya dhulma zao na jeuri zao, na kufukuza kwao kila mwenye kubainisha haki kwa watu au kunyanyua sauti yake katika kuamrisha mema na kukataza mabaya; basi walipandikiza fikra ya kumchukia kila mwenye kusema kua inafaa kumpiga vita mtawala dhalimu na kuwa mpizani wa siasa zake na vitendo vyake viovu, basi -kwa sababu hiyo- wakawabandika wapinzani wao kua ni Makhawariji waliotoka katika dini, na wakaharibu uhakika wao, basi mazushi yao

yakaenea katika vitabu vya wakati huo, na wengi wasiochunguza ukweli wakayakubali kua hayo ni sahihi, na ikafikia hali ya kukubalisha kuwaua Maibadhi (bila ya hoja isipokua kutegemea mazushi na uongo), hayo yalitokezea kwa mujibu wa fatwa za mashekhe wa watawala hao.

12. S. Ni msimamo gani wanaoufuata Maibadhi dhidi ya wasiokua Maibadhi?
J. Maibadhi ni maarufu kwa uadilifu katika misimamo yao, basi wao wamekua ni maarufu kwa kuchunguza ukweli katika hukumu zao, hayo yameptikana ni katika nyanja zote, hata katika kufuatilia madhehebu yanayopingana na wao, Maibadhi sio kama wengine wenye kuwahukumu wapinzani wao kimadhdhebu kua ni washirikina na makafiri, kisha wakatoa fatwa za kuharamisha kuoana nao, na kuhalalisha damu zao (na mali zao), hayo kwamwe hayajawahi kufanywa na Maibadhi.

13. S. Maibadhi wanawafanya vipi wasiokua maibadhi katika kivuli cha utwala wa kiibadhi?

J. Tarehe ya Maibadhi inashuhudia kua wao ni waadilifu wa kijamii. Maibadhi wanapotawala, wananchi walio wafuasi wa madhehebu mengine hufurahika kwa kupata haki zao zote za kijamii, basi haki na majukumu huwa sawa kwa wote, hali yao katika hilo ni sawa sawa na kila muislamu ikiwa ni muibadhi au si muibadhi, basi huwa pamoja nao, na kuishi nao kwa mahusiano bora na mazuri, na kama litatokezea lenye kwenda kinyume na hivyo, basi huzingatiwa kua ni dhulma (kwa mujibu wa mafundisho ya Ibadhi), basi haliwezi kukubalika katika dhehebu la Ibadhi.

BAADHI YA MASUALA YANAYOHUSIANA NA SALA KATIKA IBADHI

1. S. Kwa nini Taujihi ya sala katika Ibadhi inakua kabla ya Tak-biratu l-ih-raam?
   J. Kwa sababu Maibadhi wanategemea hadithi iliyomo katika vitabu vya Sunna, kama vile Sunan Abi daudi, Ibn maajah, Tirmidhi, Alhaakim, na wengineo kutoka kwa Bibi Aisha Mama wa waumini (r.a), kua Nabii (s.a.w) alikua anaposimama kwa kuikusudia sala alikua akisema:

((سُبْحَانَكَ اللّٰهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، تَبَارَكَ اسْمُكَ، وَتَعَالَى جَدُّكَ، وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ))

((Umetakasika Ewe Allah, na shukurani zote ni kwako, limetukuka jina lako, umetukuka utukufu wako, wala hakuna mungu isipokua wewe tu)).

Na amepokea Abu ghanim Al-khurasani (mpokezi wa kiibadhi), kua hiyo ilikua Taujihi ya Abu bakar, na Omar, na Ibn masoud, kisha wanatoa Tak-bira, kisha wanaleta Istiadha baada ya Tak-bira.

2. S. Kwa nini Maibadhi hawanyanyui mikono yao wakati wa Tak-bira ya kuhirimia katika sala?
   J. Kwa sababu wao wanategemea katika hilo yale yaliyokuja - katika hadithi nyingi - yenye kuonesha kuwepo katazo la kunyanyua mikono katika sala; kwani wamepokea Maimamu wa hadithi, miongoni mwao ni Imam Rabii (r.a), kama walivyoyapokea Maimamu tegemeo wa kisunni katika mapokezi ya hadithi kama vile Muslim, Nasaai, na Abu daudi.

3. S. Ni hadithi gani iliyokuja katika kukataza kunyanyua mikono miwili katika sala?
   J. Hiyo ni ile hadithi yenye kuthibitisha katazo la kunyanyua mikono katika sala, nayo imekuja kwa mapokezi mengi kama ilivyotangulia, miongoni mwa hayo ni pokezi la Imam Rabii (r.a): Abu ubaidah kutoka kwa Jabir bin Zaid kutoka kwa Ibn abas kutoka kwa Nabii (s.a.w) amesema:
   ((كَأَنِّي بِقَوْمٍ يَأْتُونَ مِنْ بَعْدِي يَرْفَعُونَ أَيْدِيَهُمْ فِي الصَّلاَةِ كَأَنَّهَا أَذْنَابُ خَيْلٍ شُمُسٍ))

((Kama mimi ninaona watu, watakuja baada yangu, wananyanyua mikono yao katika sala, mikono hiyo ni kama mikia ya farasi wakaidi))

[Rabii (216), (912)]

Na miongoni mwa hayo ni pokezi la Imam Muslim: Ametuhadithi Abu bakar bin Abi shaibah, na Kuraib; wamesema: Ametuhadithia Abu muawiyah kutoka kwa Aamash kutoka kwa Musayab bin Raafii kutoka kwa Tamim bin Tarafah kutoka kwa Jabir bin Samurah, amesema: Alitutokea Mtume wa Allah (s.a.w) basi alisema:

((مَا لِي أَرَاكُمْ رَافِعِي أَيْدِيكُمْ ، كَأَنَّهَا أَذْنَابُ خَيْلٍ شُمْسٍ ، اسْكُنُوا فِي الصَّلَاةِ))

*((*Vipi *mimi,* nakuoneni *ni wanye kunyanyua mikono yenu kama ni mikia ya farasi wakaidi, tulizaneni katika Sala))*

Akasema (Jabir): Kisha akatutokea na akasema:

((أَلَا تَصُفُّونَ كَمَا تَصُفُّ الْمَلَائِكَةُ عِنْدَ رَبِّهَا ؟))

((Hivi hamupangi *safu kama wanavyopanga safu Malaika kwa Mola wao?!!))*

Tukasema: "Ewe Mtume wa Allah!!, kwani vipi Malaika wanapanga safu zao kwa Mola wao?" Akasema:

((يُتِمُّونَ الصُّفُوفَ الأُوَلَ وَيَتَرَاصُّونَ فِي الصَّفِّ))

((Wanazitimiza safu za mwanzo, na wanakaribiana vizuri katika safu))

Na amenihadithia Abu al-ashajji, ametuhadithia Waqii na ametuhadithia Is-haaq bin Ibrahim ametupa khabari Issa bin Younus wote wamesema: Ametuhadithiwa Aamash kwa upokezi huu mfano wake. [Sahihi Muslim 656]

4. S. Wapinzani wa maibadhi wanasema nini kuhusu hadithi hizi zenye kukataza kunyanyua mikono katika sala?

J. Wao wamelipinga hilo kwa kusema: "kua katazo la kunyanyua mikono linazingatiwa katika hali ya kuinyanyua wakati wa kutoa salamu tu". Lakini kila mwenye kuzingatia majibu yao katika hili, anakutia kua tamko la kutoa salamu halikuja kabisa katika hadithi hii, nalo limekuja katika

hadithi nyengine, na haiwezekani kua hadithi mbili hizo ziwe katika tokeo moja, kwa hivyo hauthibiti uzingatiaji wao huo; kwa sababu udhahiri wa hadithi hii uko wazi (katika sala), nao ni kukataza kila nyanyuo la mkono katika sala, tena linaingia hata hilo nyanyuo la mkono wakati wa kutoa salamu.

5. S. Ni hadithi gani iliyojengewa usahihi wa sala kwa Maibadhi na wengine wasiokua wao?
J. Hadithi hiyo ni ile hadithi mashuhuri kwa jina la **"Hadithi ya aliyeharibu sala yake"** nayo wameipokea Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu hurairah na wengineo katika Masahaba (r.a): Kua Mtume wa Allah (s.a.w) aliingia msikitini, basi akaingia mtu na akasali, kisha yule mtu akaja kumsalimia Nabii (s.a.w), naye akamrejeshea salamu yake na akamwambia *((Rudi usali tena; kwani hakika yako hujasali))*, basi yule mtu akarudia kama alivyokua amesali, kisha akaja tena kumsalimia Nabii (s.a.w), naye akamwambia tena *((Rejea usali tena; kwani hakika yako*

hujasali)), yakawa hayo mara tatu. Basi yule mtu akasema: "Naapa kwa yule aliyekutuma kwa haki, siwezi kuboresha zaidi ya nilivyosali, basi nielimishe" hapo Mtume (s.a.w) akasema: *((Ukisimama kwa ajili ya sala, toa takbira, kisha soma kilichowepesika kwako katika Qur-ani, kisha rukuu mpaka utulizane nawe umerukuu, kisha nyanyuka mpaka utulizane nawe umesimama, kisha sujudu mpaka utulizane nawe umesujudu, kisha nyanyuka kwa kukaa kitako mpaka utulizane nawe umekaa kitako, na ufanye hayo katika sala yako yote))* [Albukhari 724, Muslim 397, Tirmidhi 279]

Hadithi hii ndiyo msingi uliojengewa usahihi wa sala, basi -kutokana na hayo- wamefikia baadhi ya wanaelimu kusema: *"Hakika yaliyotajwa katika hadithi hii ndiyo ya lazima, na yasiyokuwamo sio ya lazima"*.

Na kama ilivyobainika ndani yake (hiyo hadithi), hakika tendo la kunyanyua mikono halikutajwa katika hadithi hii, vile vile halikutajwa tendo la kuufunga mkono wa kulia juu ya wa kushoto,

basi, lau kunyanyua mikono na kuifunga -wa kulia juu ya wa kushoto- ni katika yaliyolazimika katika sala angaliyafafanua Mtume (s.a.w) kwa mtu huyu.

6. S. Inafahamika nini kuhusiana na zile hadithi zilizokuja kubainisha sifa ya sala ya Mtume (s.a.w)? nazo hazikutaja kunyanyua mikono wakati wa kutoa Takbira?
   J. Inafahamika -kwa mujibu wa hadithi hizo- kua kunyanyua mikono sio tendo la kukazaniwa katika matendo ya sala, na kua asiyenyanyua mikono pamoja na Takbira hajaenda kinyume na sunna, na wala haisemwi kua amepinga sunna kama wanavyodai baadhi yao, bali inakhofiwa kuwa mwenye kunyanyua mikono yake yumo katika kuenda kinyume na sunna; kwani limethibiti katazo la kunyanyua mikono kama ulivyoona katika dalili tulizozitaja na nyenginezo.

7. S. Jee!! zina hukumu gani zile hadithi zilizozipokelewa katika baaadhi ya vitabu vya

sunna, nazo zimethibitisha kunyanyua mikono katika sala?

J. Ikiwa imepokelewa kua Nabii (s.a.w) amenyanyua mikono yake katika sala, na ikapokelewa vile vile kua yeye (s.a.w) amekataza kunyanyua mikono katika sala, basi la busara na bora zaidi ni kushikamana na katazo; kwa sababu, katazo linatangulizwa mbele ya amri, na hili ni katika misingi ya kifiqhi iliyo maarufu, pia kwa neno lake (s.a.w):

((فَإِذَا أَمَرْتُكُمْ بِشَيْءٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ ، وَإِذَا نَهَيْتُكُمْ عَنْ شَيْءٍ فَاجتنبوه))

((Nikikuamrisheri kitu basi kifanyeni munayoyaweza, na nikikutazeni kitu basi mujiepushe nacho))

[Muslim 2388 Bukhari 6773]

Na vile vile, pamoja na wingi wa hadithi zilizokuja katika kunyanyua mikono, tunaona wanaelimu wa hao wenye kunyanyua mikono wamefafanua kua kunyanyua mikono sio sharti ya usahihi wa sala, wala sio la lazima, bali inafaa kuliacha tendo hilo, basi hilo -la kunyanyua

mikono kwa upande wao- halizingitiwi kua ni nguzo katika nguzo za sala, wala halizingatiwi kua ni katika sunna zilizotiliwa mkazo, bali hakika wanaelimu wengi wanaliorodhesha tendo hilo -la kunyanyua mikono- kua ni katika yanayopendelewa tu, kwa hakika, mja kuacha linalopendelewa ni kheri kwake kuliko kuja akafanya lililokatazwa.

8. S. Tunapata faida gani ya kielimu kutokana na mapokezi hayo (ya kunyanyua mikono) na mabainisho ya wanaelimu?

   J. Faida kubwa tunayoipata, ni kua namna ya sala kama ilivyo katika Ibadhi ndio sahihi kwa makubaliano ya Waislamu wa kila dhehebu.

   Basi Maibadhi ni wenye kutekeleza ibada ya sala kama ilivyopokelewa kutoka kwa Mtume (s.a.w), na kwa namna ambayo wanaelimu wa kiislamu -kwa madhehebu yote- wamekubaliana kua ni sala iliyotimia, na iliyokusanya nguzo zake, na shuruti zake zinanazotakiwa katika sala, bila ya kuwemo pungufu la kuibatilisha.

9. S. Maibadhi wanasema nini katika suala zima la kufunga mikono katika sala? Pia wanasema nini kuhusu mapokezi yaliyoegemezwa kwa Mtume (s.a.w) katika suala hilo?

   J. Maibadhi tokea mwanzo hawafungi mikono yao katika sala, na yamethibiti kwao, kua hadithi zilizokuja katika kufunga mikono hazina nguvu wala uwazi katika kulithibitisha tendo hilo, kua ni sunna katika sunna za sala, pia tukiwaangalia walioshikamana na msimamo wa kufunga mikono, tunawakutia wenyewe wanatafautiana katika hilo:-

a. ni wakati gani linatakiwa?
b. na namna gani linatakiwa?

   Miongoni mwao wako waliosema: Hilo ni katika sala za sunna tu.

   Na wako waliosema: Linatakiwa katika faridha na sunna.

   Na wengine wamesema: Halifanywi hilo katika faridha na katika sunna.

   Ama ni wapi ifungwe hiyo mikono?

Wako waliosema: Uwekwe wa kulia juu ya wa kushoto kifuani.

Na wengine wamesema: Iwekwe juu ya kitovu.

Na wengine wamesema: Iwekwe chini ya kitovu.

Vile vile katika kuinyanyua mikono.

Imesemwa: haliwi hilo isipokua mara moja tu.

Na imesemwa: ni katika sehemu nne tu.

Na imesemwa: linatakiwa kutendwa katika zaidi ya hizo sehemu nne....

Namna hiyo mpaka mwisho wa tofauti zao katika jambo hilo.

Kama tunavyoyaona hayo katika waliyoyapokea katika hadithi zao; kwani hakuna katika hadithi hizo hata hadithi moja iliyo sahihi na kusalimika kutiwa kasoro na utata, kama walivyoyafafanua hayo baadhi ya wanaelimu wachunguzaji wa mapokezi, nao ni wanaelimu wasiokua Maibadhi.

10. S. Yanaonesha nini hayo ya wingi wa kutafautiana kwao katika suala zima la kunyanyua mikono na kuifunga, na kugongana kwa mapokezi yao katika hilo?

J. Hayo (ya kutofautiana kwao na kugongana kwa mapokezi yao) yanaonesha kua, kunyanyua mikono na kuifunga katika sala ni jambo lisilopata daraja ya kuthibiti kua ni tendo katika matendo ya sala, au kua ni sifa iliyoshikamana na sala ya Mtume (s.a.w).

Na lau kua hayo yanapata daraja ya kukubalika; basi isingetokea tofauti hiyo na kuingia jambo hilo katika utata huo; kwa sababu, sala ilikua ni tendo alilolitenda Mtume (s.a.w) na alilodumu nalo zaidi, naye akiwa na Masahaba wake (r.a), kila siku mara tano, mchana na usiku muda wote wa miaka ya Utume wake (s.a.w).

Hakika akili haikubali, kua Masahaba (r.a) wawe hawakuhifadhi matendo ya sala kwa usanifu wa juu kabisa.

11. S. Jee!! yamepokewa yenye kuonesha kuachia mikono na kutoifunga katika sala kutoka kwa Masahaba na Matabiina?

J. Ndio, hayo yamepokewa kutoka kwa Sahaba Abdullahi bin Zubair, kua yeye alikua akiachia

mikono yake katika sala, kama alivyoyapokea hayo Ibn Abi shaibah, kama yalivyopokelewa kutoka kwa Matabiina wakubwa miongoni mwa hao ni: Said bin Musayyab, Said bin Jubair, Mujahid, Hassan Al-basri, Nakhaii, na Ibn siirin, kama alivyoyaeleza Ibn mundhir, na hayo yanaonesha, kua kufunga mikono (katika sala) hakukujuilikana kwao wao, na wao walikua zama moja na Masahaba wakarimu Allah awawie radhi.

12. S. Kwa nini Maibadhi hawaleti "Aamin" baada ya kisomo cha Al-faatiha (Alhamdu) katika sala?

    J. Kwa sababu hilo ni tamko la nyongeza, nalo halimo katika Alhamdu kwa makubaliano ya wanaelimu wote wa kiislamu; kwa maana hiyo, litakua tamko hilo (la Aamin) ni katika maneno ya watu, na sisi tumekatazwa kuingiza maneno ya watu katika sala, kama yalivyothibiti hayo kutoka kwa Mtume (s.a.w).

    Pia kwa sababu ya kutothibiti mapokezi waliyoyategemea wenye kuthibitisha kuleta "Aamin" baada ya Alhamdu; kwani uhakika wake

ni mapokezi yaliyozongwa na utata wa kudhania, basi mapokezi hayo utayakuta:-

a. ima ni dhaifu.
b. au yanagongana.
c. au ya kupachikwa (uzushi).

Vile vile, hata kama (tutakadiria) kuthibiti baadhi ya mapokezi hayo, hayatotoka nje ya hukumu ya yale yaliyotokea kabla ya kukatazwa maneno ya watu katika sala, bali amesema mwanatafsiri Ibn arabii: *"Hakuna hadithi iliyo sahihi katika kuithibitisha Aamin"*.

Pia tukizingatia kua hukumu ya kuleta "Aamin" (kwa wale wenye kuithibitisha) ni kupendelewa tu, hayo ni kwa wenye kuikubali kua ni katika matendo ya sala, na kwa hivyo (kuitikia Aamin) sio tendo la lazima.

Kwa hivyo Maibadhi wamekua katika msimamo wa usalma na yakini, na kua wao wamo katika makubaliano yaliyo wazi, (wamejiweka mbali na tofauti) wakifuata mafundisho ya ile hadithi waliyoipokea Ahmed, Shaafii, Nasaaii,

Twabaranii, Abu daudi, na wengineo kutoka kwa Ibn Masoud kua Nabii (s.a.w) amesema:
((Hakika Allah hueka katika jambo lake alitakalo, na katika aliyoyaweka ni kua musiseme katika sala)).

13. S. Kwa nini Maibadhi hawasomi chochote cha Qur-ani baada ya kusoma Alhamdu katika faradhi mbili za Adhuhuri na Al-asiri?
J. Kwa sababu wao wanategemea katika msimamo wao huo dalili nyingi, miongoni mwa hizo, ni yale waliyoyapokea wanahadithi wenyewe, kama vile upokezi wa Abu daudi katika Sunani yake, kutoka kwa Ibn abbaas Allah amridhie kua waliingia kwake nao wakamuuliza: *"Jee!! alikua Mtume wa Allah (s.a.w) akisoma katika Adhuhuri na Laasiri?"* akasema: *"Hakua akisoma"*. Ikasemwa: *"Pengine yeye alikua akisoma kwa siri?"* hapo kasema: *"Hili ni ovu zaidi kuliko la mwanzo!; kwani alikua ni mja mwenye kuamrishwa amefikisha aliyoamrishwa.."*

na ameyapokea Nasaaii mfano wa hayo.
Na pokezi hili ni la wazi na la kugogoteza, ama mapokezi yenye kuonesha kuwepo kwa kisomo cha ziada baada ya Alhamdu katika faridha mbili ya Adhuhuri na Al-asiri, hakika mapokezi hayo ni yenye kugongana kwa wazi, nayo yanaonesha kutegemea njia ya kujihukumia kwa dhana na sio yakini, na mengine yasiyokua hayo, ambayo yamewafanya Maibadhi wasifanyie kazi mapokezi hayo ya kuitikia "Aamin" baada ya Alhamdu.

14. S. Kwa nini Maibadhi wanatoa salamu moja tu wakati wa kumaliza sala?
J. Kwa sababu Maibadhi wanategemea katika hilo, hadithi iliyopokelewa katika vitabu vya Sunna, kama vile Tirmidhi, Ibn maajah, Ahmed bin Hanmbal, Twabarani, na Bayhaqii kutoka kwa Aisha mama wa waumini, na Anas bin Malik, na Salamah bin l-aq-wai, na Sahal bin Saad (r.a): *((Kua Nabii (s.a.w) alikua akitoa salamu moja))*. na walikua Muhajirina wanatoa

salamu moja.
Pia Ijulikane kua Maibadhi -vile vile- wanakubalisha kutoa salamu mara mbili, kama ilivyokua ipo khilafu kwa wasiokua Maibadhi, jee! salamu ni moja au ni mbili?! lakini Imam Nawawi amenukulu makubaliano ya kua *"hailazimiki isipokua salamu moja tu"*.

15. S. Jee!! siasa iliathiri katika mwenendo wa Fiqhi (ibada za matendo) na kuwalazimisha watu kufuata rai fulani tu?
J. Ndio, siasa ilikua na taathira zake kubwa katika kuiendesha jamii kwa mujibu wa Fiqhi (iliyokubaliana na dola), kwa hakika Dola zilizopita (hapo kabla) zilikua zikiihukumu miji ya waislamu kwa mafundisho ya dhehebu maalumu, na (kufuata siasa ya) kulazimisha kuhukumu kwa mujibu wa mafundisho ya dhehebu la dola tu. Kwa mfano dhehebu la Abu hanifa lilikua limeenea katika nchi za mashariki; kwa sababu Dola ya Abbasiyah ililifanya kua ni dhehebu lake rasmi na kulipa kila nguvu katika

mamlaka yake, na kwa upande mwengine dhehebu la Maliki lilienea katika nchi za magharibi; kwa sababu dola zilizohukumu huko zililifanya dhehebu hilo kua ndio dhehebu lake na kulipa kila nguvu, ama Faatimiyuuna kwa hakika walieneza dhehebu la Is-mailiyah walipoihukumu Misri na nchi nyenginezo, na wakazuia kusomesha dhehebu la Abu hanifa; kwa sababu lilikua ni dhehebu la dola ya Abbasiyah, ama Maumayyah katika Andulus (Spain leo) walivaa njuga za kueneza dhehebu la kimaliki, na Maayubiyuna waliingia katika njia ya kueneza dhehebu la kishafii, na juu ya kua dhehebu la Abu hanifa na dhehebu la Malik yote mawili yalikua ndio madhehebu yalioenea zaidi hapo nyuma, isipokua katika miaka ya hivi mwisho -kwa sababu ya kupata kipaumbele kwa nguvu za kimali na utangazaji katika baadhi ya madola na mashirika- utaona kuenea dhehebu la kiwahabi (Salafii) katika miji mingi ya waislamu.

KIMETIMIA
KWA
UWEZO WA ALLAH

Imetimia ratajuma ya kitabu hichi
kwa mkono wa mja fakiri mwenye kutaraji ridha za
Mola wake Allah mtukufu
By
Hafidh. H. Seif Al sawafi

leo
Jumatatu ya terehe
05/01/1434Hijria - 19/11/2012 AD

Asante sana
kwa usomaji wako
Kwa mawasiliano na mtarijimu
Barua pepe: sawafiy@hotmail.com

للطلب والحجز
٠٠٩٦٨ ٩٣٢٧٧١١٩ أو ٠٠٩٦٨ ٩٢٢٢٨١٦٦



www.noor-alestiqamah.com/vb

عن دافع التصميم والإخراج الفني
عدنان الجلندائي ٩٥٤٧١٣٤٥